# 32 Hadithi

# KATIKA ATHARI ZA KUAMINI MAKADIRIO

Kutoka kwa Ibn wa Abbaas (Radhi za Mwenyezi ziwe juu yake), amesema: Siku moja nilikuwa nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, akasema:

1. "Ewe kijana, hakika mimi ninakufundisha maneno (haya):
2. Mhifadhi Mwenyezi Mungu
3. Ili naye akuhifadhi
4. Muhifadhi Mwenyezi Mungu utampata mbele yako (kwa kila jambo lako)
5. Pindi utakapoomba, muombe Mwenyezi Mungu
6. Na ukitaka msaada basi taka msaada kwa Mwenyezi Mungu
7. Tambua kwamba jamii ikikubaliana kukusaidia kwa lolote, haiwezi kukusaidia ila jambo ambalo Mwenyezi Mungu amekuandikia, na lau ikikubaliana ikudhuru kwa lolote, haiwezi kukudhuru ila kwa jambo ambalo Mwenyezi Mungu amekuandikia.
8. Kalamu imeshanyanyuliwa na karatasi zimesha kauka. [1]

1 Al-Tirmidhiy (2516), na amesema: Ni Hadithi nzuri, na sahihi, na Abd al-Haqq ameisahihisha katika "Al-Ahkam Al-Wusta" (4/285).

## Ayah

Amesema Mwenyezi Mungu

*﴿Wewe tu tunakuabudu, na wewe tu tunakuomba msaada﴾ [Al-Fatihah: 5].*

*﴿Na timizeni ahadi yangu, na Mimi nitatimiza ahadi yenu, na niogopeni Mimi tu." [Al-Baqarah: 40].*

*Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:*

*﴿Na Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea ila Yeye. Na akikutakia kheri, basi hapana awezaye kurudisha fadhila yake﴾ [Yunus: 107].*

*﴿Hayo hivyo ni kwa ajili tumuepushe na uovu na uchafu. Hakika yeye alikuwa katika waja wetu walio safishwa﴾ [Yusuf: 24].*

*﴿Na Mola wenu Mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni". [Ghafir: 60].*

*﴿Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi﴾ [Al-Hadid: 22].*

## Msimulizi

Ni Abul Abbaas, Abdullah bin Abbaas bin Abdul muttwalib, kabila lake ni Quraish, ukoo wa Hashim, amezaliwa kwenye mtaa wa ukoo wa Hashim miaka mitatu kabla Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) hajahamia Madina, ni katika wasomi wakubwa wa Umma huu na ni mfasiri wa Qur`Ani, Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alimuombea dua kwa kauli yake: "Eh Mwenyezi Mungu mjalie maarifa ya kuijua dini"[1] na ni katika maswahaba (wanafunzi wa Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake)) walio pokea hadith nyingi, alisilimu akiwa mdogo na aliishi na Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) baada ya vita vya ufunguzi wa Makka, alipofuka mwishoni mwa umri wake, alifia Twaif mwaka 68H[2]

## Muhtasari

Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) anamnasihi Mtoto wa ami yake Abdullah bin Abbaas kwa usia ulio kusanya tauhiid ya uluuhiyyah (kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu mmoja tu) kwamba asiombwe yeyote katika maombi ila yeye pekee, na wala asitake msaada kwa yeyote ila yeye pekee. Anauandaa moyo wake kwa kumwambia kwamba mambo yote yako katika mipango ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kwa hakika hayupo yeyote anayeweza kumnufaisha au kumdhuru ila kwa jambo ambalo amelipanga.

1 Al-Bukhari (143) na lafudhi ni yake, na Muslim (2477).

2 Rejea ufafanuzi wake katika: "Maarifaat al-Sahaba" cha Abu Naim (3/1699), ""aliastieab fi maerifat al'ashabi"" cha Ibn Abd al-Barr (3/933), "Asad al-Ghaba" cha Ibn al- Athiri (3/291).

# Ufahamu

Ibn Abbaas (Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) alikuwa nyuma ya Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) wamepanda mnyama.

1 Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akataka amfundishe somo linalo husu kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ili kuvuta usikivu na akili yake, akumuita kulingana na umri wake, alikuwa ni kijana mwenye umri wa miaka kati ya kumi hadi kumi na nne, akamwambia: "hakika mimi ninakufundisha maneno" akimaanisha: uyahifadhi, uyaelewe na uyafanyie kazi.

2 Jambo la kwanza alilomfundisha ni, amuhifadhi Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kuto vunja mipaka aliyoiweka na kutekeleza aliyoamrisha, aamrishe aliyomuamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu na akataze aliyomkataza. amesema Mwenyezi Mungu: " Na wanaolinda mipaka ya Mwenyezi Mungu ". [At-Tawbah: 112] Amesema Mwenyezi Mungu: 32. "Haya ndiyo mnayoahidiwa kwa kila mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu na akajilinda.33. Mwenye kumwogopa Mwingi wa Rehema hali yakuwa hamwoni, na akaja kwa moyo ulioelekea" [qaaf: 32, 33].

3 Mwanadamu anapo hifadhi mipaka ya Mola wake na akatekeleza maamrisho yake, atalipwa kwa matendo yake, kama anavyomuhifadhi Mwenyezi Mungu Mtukufu, pia Mwenyezi Mungu Mtukufu anamuhifadhi. Hifadhi ya Mwenyezi Mungu inajumuisha kuhifadhi mwili, viungo, akili na vinginevyo. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Kila mtu analokundi la malaika mbele yake na nyuma yake linamlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu." [ra`ad: 11],.

Hifadhi ya Mwenyezi Mungu haikomei kwa huyu anayehifadhi mipaka yake tu, bali humuhifadhia familia yake pia, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na wachelee wale ambao lau kuwa na wao wangeliacha nyuma yao watoto wanyonge wangeliwakhofia. Basi nao wamche Mwenyezi Mungu, na waseme maneno yaliyosawa.". Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:" Na baba yao alikuwa ni mtu mwema.".

Na daraja la juu la Mola kumuhifadhi mja wake ni kumuhifadhia dini yake, kumuhifdhi dhidi ya wasiwasi na mienendo ya shetani, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Hayo ni kwa ajili ya kumuepusha na uovu na uchafu. Hakika yeye alikuwa katika waja wetu walio safishwa. [Yusuf: 24]. Na ndio maana amesema Ibn Abbaas akitafasiri Kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa." [Al-Anfal: 24]:, Anamkinga muumini dhidi ya maasi ambayo yatampeleka Motoni.[1]

1 Tazama: "Jami' al-Ulum wa al-Hakam" cha Ibn Rajab (1/470).

4 Kisha Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akataja malipo mengine ya anaye hifadhi mipaka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, nayo ni Mwenyezi Mungu kuwa naye Maisha yake yote, anamsaidia, anamlinda, anampa nguvu, anamjibu maombi yake na anakubali ibada zake; amesema Mtume Mtukufu, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Na mja anapo endelea kujiweka karibu na mimi kwa kutekeleza ibada za Sunna, (za hiyari) mpaka ninampenda, nikimpenda, ninakuwa sikio lake analotumia kusikia, na jicho lake analotumia kuona, na mkono wake anaotumia kushika, na mguu wake anaotumia kutembea, na akiniomba kwa hakika ninamjibu, na akinitaka ulinzi kwa hakika ninamkinga “ .[1]

5 Kisha Mtume Mtukufu akamuelekeza mlango Mtukufu katika milango ya Tawhiid na itikadi sahihi, nao ni kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake, na katika maombi asimuombe yeyote zaidi yake, kwa sababu dua ni ibada, haitakiwi kuielekeza kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, amesema Mtume S.A.W: “Dua ni ibada” kisha akasoma: “Na Mola wenu Mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni. Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia katika Jahannamu hali ya kudhalilika.” [Ghafir: 60] [2], kwa sababu katika dua kuna kudhihirisha udhalili na uhitaji wa muombaji, lakini pia kukiri kwamba anaye ombwa ana uwezo wa kuleta manufaa na kuzuia madhara, na haifai kujidhalilisha ila kwa Mwenyezi Mungu pekee; kwa sababu hiyo ndio ibada ya kweli.[3]

6 Kisha Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akamuamrisha awe anamuomba msaada Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee. Kuomba masaada; ni uhitaji wa msaada ili kufikia malengo. Kuomba msaada ni kudhihirisha jinsi unavyomtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tawhiid katika kuomba msaada tumejifunza katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: Wewe tu tunakuabudu, na wewe tu tunakuomba msaada “[Al-Fatihah: 5]. kwa sababu alipowaamrisha waja wake wamtii, aliwaelekeza wamuombe yeye pekee, na wamuombe awaongoze waache maasi na wafanye ibada.[4]

Ieleweke kwamba, kumuomba msaada kiumbe katika jambo analoliweza inaruhusiwa. Mwanadamu anaweza kumuomba mwanadamu mwenzake amsaidie kubeba mzigo au amsaidie jambo ambalo kwa kawaida mwanadamu analiweza. Inapendeza kwa mwislaam kusaidia jambo ambalo analiweza, Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) amesema:

1 Al-Bukhari (6502), kutoka kwa Abu Hurairah

2 Abu Dawood (1479), al-Tirmidhiy (3247), na al-Nasa’i katika “Al-Sunan al-Kubra” (3828), na al-Tirmidhiy amesema: Ni nzuri na ni sahihi.

3 Tazama: “Jami’ al-Ulum wa al-Hakam” cha Ibn Rajab (1/481).

4 Tazama: “nur aliaqtibas fi wsyat alnby, liibn Abbas” cha Ibn Rajab (uk. 93).

"Na ukimsaidia mtu, kwa kumbeba juu ya mnyama wake, au kumsaidia kupakia mzigo wake ni sadaka"[1]. Kuomba msaada ambako ni haramu, ni katika vitu ambavyo haviko katika uwezo wa anayeombwa, bali anaviweza Mwenyezi Mungu pekee, kama kuwaomba maiti, kuomba kwa kupitia makaburi ili upone maradhi au ufaulu mtihani au upate mtoto, kufanya hivyo ni haramu.

7 Kisha Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akamfundisha Ibn Abbaas kusalenda, kuridhia mipango ya Mwenyezi Mungu na kumtegemea kiukweli, kwa sababu mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na yote yanayo msibu mja, mabaya au mazuri yanatoka kwake, ameandika yampate kabla hajaumba mbingu na Ardhi. Hata kama viumbe wakikubaliana kuzuia alililoliandika limpate, hawawezi kufanikisha, na hata wakikubaliana kumnufaisha au kumdhuru kwa jambo ambalo hajaliandika, mipango yao haiwezi kufaulu hata kidogo. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea ila Yeye. Na akikutakia kheri, basi hapana awezaye kurudisha fadhila yake" . [Yunus: 107].". Ibara hii ndio imebeba ujumbe wa usia huu, kwa sababu mja anapotambua kwamba halimpati lolote ila alililoliandika Mwenyezi Mungu, na kwamba juhudi za viumbe hazina nafasi, hilo linamfanya amtegemee Mwenyezi Mungu Mtukufu kiukweli, ajisalimishe mbele yake, atekeleze maamrisho yake na kuacha makatazo, aidha kuipa kauli yake kipaumbele zaidi kuliko kauli yoyote, na haogopi wala hamuombi yeyote zaidi yake.[2]

8 Kisha Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akaeleza kwamba kalamu zilizoandika mambo yote yatakayo wapata viumbe zimezuiliwa kuandika, na vitabu vilivyoandikwa yamethibitishwa yote yaliyoandikwa, hakuna marekebisho. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: " Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi". [Al-Hadid: 22]. Na "Mwenyezi Mungu Mtukufu ameandika mambo yote yatakayowapata viumbe miaka hamsini elfu kabla hajaumba mbingu na Ardhi"[3]

1 Al-Bukhari (2989), na Muslim (1009), kutoka kwa Abu Hurayrah.

2 "Jami' al-Ulum wa al-Hakam" cha Ibn Rajab (1/484).

3 Muslim (2653).



# Mafunzo

1. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alikuwa anatumia muda wake na wa maswahaba zake kwa kumtii Mwenyezi Mungu, hata wakiwa wamepanda mnyama..

2. Shauku ya Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) ya kumfundisha Ibn Abbaas japo ni mdogo kiumri, hadith yenye maana pana katika upande wa mwenendo, tawhiid na mambo yanayotusibu na mengine mengi, hii inatufundisha kwamba haifai kuwapuuza watoto, hasa waelevu, lakini pia kila mmoja afikishiwe kwa lugha inayoendana naye, hasa katika kufundisha mambo muhimu katika dini, kwani hao ndio vijana wa kesho na ndio nguzo ya jamii kutengemaa

3. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) ameanza mazungumzo yake kwa kumuita na kumvuta msikilizaji, ni maneno machache na yenye maana pana, jambo ambalo linamfanya mtu kuwa makini na hili ni jambo ambalo linatakiwa kwa kila mwenye kutoa nasaha alizingatie. Afungue nasaha zake kwa jambo lenye kumfanya mpokeaji kuzitamani nasaha zake.



4. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) hakurefusha usia wake, bali yalikuwa ni maneno machache, hilo linapelekea kufahamika na kufanyiwa kazi, hasa kwa watoto.

5. Kama kweli unajipenda, basi muhifadhi Mwenyezi Mungu Mtukufu ili naye akuhifadhi, wamesema baadhi ya wema waliotangulia: “Mwenye kumcha Mwenyezi Mungu, amejihifadhi mwenyewe, asiyemcha amejipoteza mwenyewe na Mwenyezi Mungu hana shida naye”[1]. Hata kama unahitaji kuhifadhi afya yako, basi muhifadhi Mwenyezi Mungu Mtukufu, kuna mwanazuoni alifikisha zaidi ya miaka mia moja lakini bado alikuwa na neema ya nguvu na akili, siku moja katika matembezi akakutana na mtaro akauruka kwa nguvu, wanafunzi wake wakashangazwa sana, kwa umri wake na jinsi alivyoruka, akasema: viungo hivi tumevihifadhi dhidi ya maasi tukiwa wadogo, Mwenyezi Mungu akavihifadhi tulipokuwa wakubwa[2].



1 “Nur Aliaqtibas Fi Wsyat Alnby Liabn Ebbas”Kwa Ibn Abbas” cha Ibn Rajab (uk. 54).

2 Tazama: “Jami’ al-Ulum wa al-Hakam” cha Ibn Rajab (1/466).

# Mafunzo

6 Imepokelewa kwamba kuna mwanamke alitoka kuelekea vitani pamoja na waislaam, akaacha mbuzi kumi na mbili na kifaa alicho kuwa akikitumia kushona, aliporudi hakukuta mbuzi wala kifaa chake cha kushonea, akasema: Eh Mola wangu, hakika umechukua dhamana ya kumuhifadhia yeyote anaetoka kwa ajili ya Dini yako, na mimi nimepoteza mbuzi wangu na kifaa changu cha kushonea, nakuomba Mola wangu unirejeshee mbuzi na kifaa changu", alikuwa akimuomba Mola wake mara kwa mara, alipoamka akakuta mara mbili ya mbuzi zake na vifa viwili"[1]

7 Mja anapotaka hifadhi yake, ya familia na mali zake, basi amche Mwenyezi Mungu Mtukufu, amesema Ibnul Munkadir -Mwenyezi Mungu amrehemu-: "Hakika Mwenyezi mungu humuhifadhia mtu mwema mwanae, mjukuu wake na nyumba zinazomzunguka, wanakuwa katika himaya na sitara yake"[2]. Na Said bin Musayyib -Mwenyezi Mungu amrehemu- alimwambia mwanae: (mimi ninairefusha sala yangu kwa matarajio ya kukuhifadhi, akasoma maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yasemayo: " Na baba yao alikuwa ni mtu mwema. [kahf: 82][3]

8 Namna za kuomba na kuabudu viumbe zinaibuka mpya kila kukicha, kama kuomba nguvu za kiulimwengu au wazazi baada ya kifo. Mfano wa hayo ni filam, vinyago vya kuchezea watoto na semina zenye kujihusisha na imani za kipagani. Kuwa makini, ushirikina unaibuka ukiwa na majina tofauti.

9 Jiepushe na ibada ya kuomba viumbe hata kama ni kidogo, na ujizoeshe kujihudumia mwenyewe, Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alichukua ahadi ya kiapo kwa baadhi watu juu ya mambo kadhaa, miongoni mwa mambo hayo ni: " Na wala msiwaombe watu chochote", mpokeaji wa hadith hii amesema: nilimuona mmoja wao, fimbo yake inadondoka akiwa juu ya mnyama, na wala hamuombi yeyote amuokotee[4], jambo hili hata kama si haramu, lakini ni msukumo wa tabia njema na kujitunzia heshima kwa kuepuka masimango ya wanadamu, aidha kujifunza tabia ya uvumilivu katika kipindi cha shida, pia kujitunzia heshima na kutohitaji misaada ya watu. Walipo kula kiapo, walitekeleza hata katika mazingira ambayo si makusudio yake, ili kufunga milango na njia zote zenye kupelekea kukivunja.[5]

1 Ahmad katika "Musnad" yake (34/260), (20664), na al-Haythami aliiweka daraja kuwa ni sahihi katika "Majma' al-Zawa'id na Manbi' al-Fawa'id" (5/277).

2 "Jami' al-Ulum wa al-Hakam" cha Ibn Rajab (1/467).

3 "Jami' al-Ulum wa al-Hakam" cha Ibn Rajab (1/467).

4 Muslim (1043).

5 Al-Mufhim cha Al-Qurtubi (3/86).

10 Omba msaada kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa mambo yenye kukunufaisha katika Dini na Dunia yako, kama kudumisha Sala, kuwa na tabia njema, katika masomo na kutafuta kazi, hakuna chenye nguvu kuliko kumuomba Mwenyezi Mungu msaada, Mtume Mtukufu amekuuusia: "pupia kufanya lenye kukunufaisha na umuombe Mwenyezi Mungu msaada"(1) kithirisha kumuomba Mwenyezi Mungu msaada, Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alimwambia Muadh bin Jabal: "nakuusia ewe muadh, usiache kusema mwisho wa kila sala: Eh Mwenyezi Mungu nakuomba unisaidie niwe nakutaja, kukushukuru na kukuabudu kwa Ufanisi"(2)

11 Ni kwa kiasi gani tunawategemea viumbe? Na ni kwa kiasi gani tunamtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu?. Wahabu bun Munabbih -Mwenyezi Mungu amrehemu- alimwambi mtu aliye kuwa akienda kwa wafalme: "una nini! Unaenda kwa mtu ambae anafunga mlango wake na kukuacha nje, ana kuonyesha kwamba ni fukara, na anaficha utajiri wake, unamuacha ambae anafungua mlango wake nusu ya usiku na nusu ya mchana, na anakuwekea wazi utajiri wake, anakwambia: niombe, nami nitaitikia maombi yako"(3)

12 Kuwa na shauku ya kujifunza hadith hii, kuifanyia kazi, na kumfundisha mkeo,mwanao na watu wengine, kila mmoja kulingana na lugha, umri na utayari wake, kwa sababu imebeba usia mzito, kiasi cha baadhi ya wanazuoni kusema: nimeisoma kwa mazingatio hadith hii ikanishangaza karibia nipagawe, ni msiba mkubwa kutoijua hadith hii, na kuielewa kwa juu juu!(4)

13 Amesema mshairi: usimuombe mwanadamu akutatulie matatizo***muombe ambae milango yake haifungwi Mwenyezi Mungu anachukia usipomuomba***na mwanadamu akiombwa anachukia.

1 Muslim (1043).
2 Abu Daawuud (1522), an-Nasa'i (1303), na an-Nawawii ameiweka daraja ya sahihi katika "Khulas al-Ahkam" (1/468).
3 "Jami' al-Ulum wa al-Hakam" cha Ibn Rajab (1/481).
4 "Jami' al-Ulum wa al-Hakam" cha Ibn Rajab (1/462).

